Wizara ya afya yajipanga Kuhudumia wageni mkutano Wa nishati jijini Dar .Uk.3

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2513 JUMANNE JANUARI 28, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# DKT SAMIA ATAKA UMEME KUFIKIA MEGAWATI 4000

>> **Anataka** Tanzania iwe mfano ifikapo 2025

>> **Rais** wa Benki ya Dunia akiri Afrika itawezekana Uk.2



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amekutana na kuzungumza na Rais wa Taasisi ya Rockefeller Dkt. Rajiv Sha Ikulu Jijini Dar es Salaam jana tarehe 27 Januari, 2025.*

## Wakulima wafagilia Ruzuku ya pembejeo ya Dkt Samia

NA MWANDISHI WETU

KUFUATIA mabadiliko makubwa katika sekta ya Kilimo na hasa uwepo wa mkazo wa serikali ya Awa,mu ya Sita katika usambazaji wa pembejeo za kilimo pamoja na kutoa mbolea ya ruzuku kumeleta matumaini makubwa kwa wakulima, katika maeneo mengi ya Tanzania.

Gazeti hili lililopiga kambi katika Kijiji cha Amani Makolo, wilayani Mbinga

>> Inaendelea Uk. 3

## Wajumbe mkutano wa nishati wavutiwa maendeleo Tanzania

Uk.3



# DKT SAMIA ATAKA UMEME KUFIKIA MEGAWATI 4000

NA MWANDISHI WETU

NIA ya Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan ni kuona nchi inajitoshelaza kwa nishati ya umeme, ambapo dhamira yake ni kuhakikisha vyanzo vyote vilivopo nchini vinafikisha idadi ya Megawati 4,000 mwaka 2025.

Hayo yamewekwa wazi na Naibu waziri Mkuu na waziri wa Nishati Dkt Doto Biteko, alipoeleza mpango wa Tanzania kuimarisha muunganiko wa Afrika kwa kuwa na Nishati safi ya kupikia.

Amesema kuwa, Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika kukuza upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani Afrika, jitihada ambazo zimeungwa mkono na mkakati wa kitaifa na kujumuishwa katika Azimio litakalotiwa saini katika mkutano huu, huku akitoa wito wa ahadi na ushirikiano zaidi katika kuboresha upatikanaji wa suluhisho la nishati safi ya kupikia barani mwetu.

Aidha, amesisitiza kuwa ifikapo mwisho wa mwaka 2025, uwezo wa Tanzania kuzalisha umeme utaongezeka hadi megawati 4,000, nishati inayotoka kwenye vyanzo safi na mbadala inavyonufaisha wakazi wa vijijini na mijini, huku miundombinu ya umeme ikifikia vijiji vyote 12,318 nchini.

Alisema Tanzania inaimarisha muunganiko wa Afrika kwa kuwa na miundombinu ya umeme inayounganisha nchi za Kenya, Burundi, Rwanda, na Uganda, huku miundombinu ya kuunganisha Zambia ikiwa inaendelea.

Pia alitaja miongoni mwa mambo mengine yatakayofanyika katika mkutano huo kuwa ni kushirikishana uzoefu; kupata ahadi muhimu za kisiasa; kutumia ushirikiano ili kufungua uwekezaji wa sekta binafsi; kuanzisha ushirikiano wa kufadhili miundombinu ya nishati; na kukubaliana mfumo wa ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Kiashiria cha Ufuatiliaji wa Maazimio ili kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa kwenye Mkutano huo.

Ametwataka viongozi walioshiriki mkutano huo kutumia fursa hiyo kuhitimisha Maazimio yanayoendana na matarajio ya bara la Afrika ya nishati na kuimarisha ushirikiano unaohitajika katika kuyatekeleza.

"Ni matarajio yangu kwamba, mamlaka zinazohusika za nishati katika kila nchi ya majaribio zitajitahidi kuhakikisha maazimio ya nishati yanafanikishwa kupitia malengo na mipango ya hatua zinazolenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme, matumizi ya nishati safi ya kupikia, nishati mbadala na mchango wa mtaji wa sekta binafsi katika kufanikisha upatikanaji wa nishati", amemalizia Dk Biteko.

Kwa upande wake Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga amesema kuwa Bara la Afrika linaweza kubadilisha sura ya Afrika kwa kuwa na juhudi za pamoja za kuunganisha rasilimali zilizopo kuhakikisha nishati ya umeme inawafikia wananchi wengi zaidi Afrika ifikapo 2030

Nae Rais wa Benki ya Afrika (AfDB), Dk Akinumwi Adesina ameipongeza nchi ya Tanzania kwa kuwa mfano wa kuigwa kwa kufanya vizuri katika uwekezaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwafikishia nishati ya umeme wananchi katika vijijini vyote 12,318.

Mkutano huo umewakutanisha Mawaziri wa Nishati, Viongozi wa Taasisi za Kimataifa za Kifedha, Wataalam na Wadau wa Mashirika ya Kiraia ambao watapata fursa ya kujadili na kukubaliana malengo, vipaumbele vya sera, suluhisho, na ahadi za jinsi ya kutekeleza Mpango wa Mission 300.



# WAJUMBE MKUTANO WA NISHATI WAVUTIWA MAENDELEO TANZANIA

NA MWANDISHI WETU

MIUNGONI mwa viongozi mbalimbali waliowasili katika Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa Nishati Afrika, wameeleza kuvutiwa na maandeleo ya nchi ya Tanzania yanayozidi kuimarika kila siku.

Tanzania imepokea zaidi ya Marais 25 na Mawaziri 60, katika mkutano huo ulioanza jana ambao unatarajiwa kumalizika leo, huku ajenda ikiwa ni kushirikiana kwa pamoja ili kuimarisha juhudi za kukabiliana na changamoto za nishati Barani Afrika.

Katika mkutano huo pia alihudhuria Rais wa Nigeria Bola Ahmed Tinubu aliyewasili na kupokelewa na Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Mahmoud Thabit Kombo.

Katika mazungumzo yao pamoja na mambo mengine alisifu juhudi kubwa za maendeleo ya Tanzania katika kipindi hiki cha uongozi wa Awamu ya sita chini ya Dkt Samia Suluhu Hassan.

Kulingana na wajumbe waliohudhuria mkutano huo mambo ya kuvutia yanayotajwa na wageni wengi ni kuwepo na utulivu na amani, pia masuala ya utalii ambayo kwa sasa yamepiga hatua kubwa hapa nchini.

Kuna matarajio makubwa baada ya msafara huu kurejea katika nchi zao, Tanzania itaanza kupokea watalii wengi watakaopata taarifa njema kutoka kwa wageni hawa waliokuwepo nchini kwa siku mbili za mkutano huo.

Kwa upande mwingine Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko amesema kuwa Tanzania inachukulia mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika (Misheni 300) kuwa ni kichocheo cha utekelezaji wa Sera yake ya Taifa ya Nishati ya kuendeleza nishati na uhifadhi.

Dk Biteko aliwaambia wajumbe wa mkutano huo jana Januari 27, 2025 wakati akifungua Mkutano huo unaofanyika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere Jijini Dar es Salaam kwa siku mbili, kuanzia leo Januari 27 hadi 28, 2025 ambapo majadiliano ya leo yamehusisha ngazi ya ukijumuisha Mawaziri na Wadau wa Nishati na Fedha na kesho mkutano huo utahusisha ngazi ya viongozi wakuu wa nchi za Afrika.

Alisema maendeleo ya nishati tunayojivunia, bado nchi inahitaji uwekezaji zaidi katika sekta ya nishati kwani matarajio yake ni kukuza shughuli za kiuchumi hususan katika sekta za viwanda, madini na huduma za ukarimu jambo ambalo linahitaji uwekezaji wa kimkakati zaidi katika sekta ya nishati.

# WIZARA YA AFYA YAJIPANGA KUHUDUMIA WAGENI MKUTANO WA NISHATI JIJINI DAR

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI mwenye dhama Afya, Mhe. Jenista Mhagama, jana alifanya ziara hospitali Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), na Hospitali ya Agakhan ili kukagua utayari wa kutoa huduma kwa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Mkutano wa Nishati unaoendelea Jijini Dar es Salaam kuanzia jana tarehe 27 hadi 28 Januari, 2025.

Mhe. Mhagama katika ziara hiyo alieza kuridhishwa kwake na juhudi za hospitali hizo kwa kuwa tayari kutoa huduma za aina yoyote endapo itatokea Kiongozi yoyote atapata changamoto itakayohitaji.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi alisema kuwa hospitali hiyo imejipanga vizuri kupitia Idara ya Tiba na Magonjwa ya Dharura ambayo ndiyo yenye watalaam wabobezi katika eneo hilo na kubwa kulizo zote nchini kuhakikisha inatoa huduma kwani ndiyo itakuwa inapokea wageni hao, kuwaimarisha na kisha kuwasambaza katika hospitali nyingine kulingana na shida aliyo nayo mgonjwa endapo itahitajika kufanya hivyo.

Mkutano wa Nishati Afrika una kauli mbiu ya Kuharikisha Upatikanaji wa Nishati Afrika, umeandaliwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania, Benki ya Dunia, Benki ya Afrika ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Marais wa Nchi za Afrika 24, wawakilishi wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika 21, Wakuu wa Taasisi za Kimataifa 6, Washirika wa Maendeleo 5 watashiriki mkutano huo ambapo pia washiriki wengine 2,600 ndani na nje ya Tanzania wamejisajili kushiriki mkutano huo.



# ZANZIBAR YAPEWA MBINU UNUNUZI WA UMMA

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande ametoa wito kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzabar kujenga Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa kutumia wataalam wa ndani ili kusimamia kikamilifu fedha za Serikali zinazotumika katika ununuzi.

Alitoa wito huo jijini Dodoma alipokutana na kufanya mazungumzo na Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyotembelea Mamlaka ya Ununuzi wa Umma nchini (PPRA) kwa ajili ya kujifunza masuala ya ununuzi wa umma kwa ujumla.

Alisema Mfumo huo pia utasaidia kurahisisha mchakato wa ununuzi pamoja na kuongeza uwazi wa zabuni kwa kujua thamani halisi ya fedha.

Aidha Mhe. Chande aliipongeza Kamati hiyo kwa kufanya uamuzi wa kuja kujifunza PPRA katika kipindi hiki ili kwenda kuboresha Muswada wa Sheria ya Ununuzi ambao utajadiliwa katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

“Haya ni maamuzi sahihi kwa sababu Taasisi za Umma ndio ambazo zinatumia bajeti kubwa katika ununzi wa umma kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Bajeti zetu zinakwenda kwenye ununuzi, kwa hiyo tunapoenda kupitisha Mswada wetu tuhakikishe Sheria imewekwa vizuri ili kuepuka changamoto”, aliongeza Mhe. Chande.



Aliwakaribisha kutembelea PPRA mara kwa mara kwa ajili ya kuendelea kujifunza zaidi na ikiwezekana waende jijini Arusha ambako kumesimikwa Mfumo wa Ununuzi ili waone uhalisia uliopo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma alisema kwa sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya maboresho ya Sheria ya Ununuzi, hivyo kamati imeamua kuja kujifunza ili waweze kuishauri Serikali kikamilifu.

“Kama nilivyosema hapo awali, hii ni Kamati ya Bayeti na kazi yeke ni kupitisha Bajeti ya Serikali ambayo ndani yake kuna miradi na kwenye miradi kuna ununuzi, kwa hiyo tumeamua tuje tuone wenzetu wanafanyaje, Sheria zao zikoje, ili tuone namna bora ya kuishauri Serikali”, aliongeza Mhe. Mwanaasha.

Naye Naibu Waziri wa Ofisi ya Raisi, Fedha na Mipango, Zanzibar, Mhe. Juma Makungu Juma, alisema wamekuja kujifunza kwa sababu fedha nyingi za Taifa zinatumika katika ununuzi hivyo ni muhimu Serikali ihakikishe fedha hizo zinatumika vizuri.

Alisema kuwa wamekuja kuchukua uzoefu wa taratibu mbalimbali za ununuzi pamja na mafanikio kwa sababu taratibu hizo za zinatofautiana kati ya Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na kujadili mafanikio na changamoto zilizopo katika masuala ya ununuzi.

# Waaipongeza seikali Awamu ya Sita kuboresha huduma za Afya

NA MWANDISHI WETU




SERIKALI imeendelea kuboresha mifumo ya Afya ikiwemo kujenga Hospitali, Vituo vya afya, Zahanati na pia kutoa vifaa tiba kwa katika maeneo mbalimbali ikiwa ni juhudi na msisitizo wa Rais wa Awamu ya Sita Dkt Samia Suluhu Hassan, ambaye tangu alipoingia madaraka aliweka msisitozo wa kuboresha maeneo hayo.

Kufuatia maboresho hayo wananchi wameendelea kufaidika na huduma hizo za tiba na kutoa shukurani kwa serikali ambayo kila uchao imekuwa ikisikiliza kero za wananchi na kujzitafutia ufumbuzi.

Hivi karibuni Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amekabidhi vitendea kazi kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii vyenye thamani ya Shilingi Milioni 674.3 kwa mikoa Saba ambayo ni Njombe, Pwani, Kigoma, Ruvuma, Songwe, Lindi pamoja na Kagera.

Waziri Mhagama amekabidhi vitendea kazi hivyo leo Januari 3, 2025 akiwa mkoani Kagera, mkoa ambao umewakilisha mikoa mengine Sita itakayotoa huduma za afya kwa wananchi ikiwemo elimu juu ya magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya milipuko.

"Vitendea kazi vilivyokabidhiwa ni pamoja na viatu maalum vya kazi, miamvuli, mabegi pamoja na sare maalum zitakazowatambulisha kuwa wao ni wahudumu wa afya ngazi ya jamii watakaokuwa wawili katika kila kitongoji (mwanamke na mwanaume)," amesema Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama alisema, mpango huo wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni mpango wa Taifa unaoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lengo likiwa ni kuhakikisha hadi ifikapo mwaka 2028 Tanzania inakuwa na wahudumu hao wapatao 137,294 nchi nzima ili kupunguza magonjwa.

Aidha, Waziri Mhagama alisema katika kipindi kifupi cha uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassa, Serikali imewezesha uwepo wa dawa pamoja na vifaa tiba ikiwemo vifaa vya uchunguzi ambavyo vinatumia tekinolojia ya hali ya juu.

"Sasa hivi kuna ongezeko la mashine ya uchunguzi wa magonjwa MRI 14, CT-Scan 45, Digital X- Ray 439, Ultrasound zaidi ya 600 pamoja na Pet-Sacan 1 mpya yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 18 ambayo tumeifunga pale kwenye Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa ajili ya wagonjwa wa kansa," amesema Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama alisema vifaa hivyo vinahitaji wataalam wabobezi, hivyo Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa Shilingi Bilioni 30 ili kusomesha wataalam bingwa na wabobezi katika masuala ya afya ikiwemo madaktari bingwa wa mionzi na usingizi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Hajat Fatma Mwasa ameishukuru Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Sekta ya Afya kwa uendelea kuboresha miundombinu pamoja na upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba ambavyo vimeweza kuwahudumia wananchi wa mkoa huo katika masuala ya afya.

"Hospitali yetu ya Rufaa ya Bukoba inapokea wagonjwa zaidi ya 300 kwa siku kwakuwa tunao madaktari bingwa 12 wanaokidhi katika fani mbalimbali, tunatoa shukurani za dhati kwa Mhe. Rais Dkt. Samia kwa kuimarisha huduma za afya kwa wagonjwa ikiwemo wagonjwa mahututi, na kwa sasa hospitali yetu inatoa huduma kama zinazotolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili," amesema Mhe. Mwasa.



# Dkt Samia apongezwa kuifungua Kigoma Kielimu

NA MWANDISHI WETU



LICHA ya Rais wa Tanzania Awamu ya Sita Dkt Samia Suluhu Hassan, kuendelea kupongezewa kutokana na kusimamia vizuri maeneo mbalimba ya maendeleo ya Watanzania, safari hii akipata pongezi kutoka mkoani Kigoma.

Hiyo imetokana na mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana tangu alipoingia madarakani, kiasi cha Tanzania kuonekana ni nchi inayopiga hatua kimaendeleo ya haraka kaika maeneo mengi.

Katika hatua ya hivi karibuni Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amepongezwa kwa kutoa fedha kiasi cha shilingi milioni 603.8 zilizofanikisha ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya Luhunga iliyopo Kijiji cha Mgombe Kata ya Nyakitonto Halmashauri ya Wilaya Kasulu.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Isaac Mwakisu alipofanya ziara shuleni hapo na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo ambayo watoto wa kidato cha kwanza tayari wameshaanza masomo.

“Napenda kutoa shukrani kwa Mhe. Rais kwa kazi kubwa ya kuifungua Kigoma kwa kuiwezesha miundombinu mbalimbali lakini leo nitaongelea shule hii mpya ya Luhunga kupitia kiasi cha shilingi milioni 603.8 alichotoa ,” ameeleza Kanali Mwakisu. Ameongeza : “ kilichonifurahisha madarasa tayari yameshakamilika na watoto tayari wapo darasani tokea Januari 13,2025 mwanzo walifikia shule mama ya Nyakitonto na leo wapo hapa ikiwa miundombinu ya kuwawezesha kukaa na kusoma ikiwa tayari,” amesema.

Pia, Kanali Mwakisu amewapongeza wasimamizi wa mradi huo kwa kushirikiana na wahandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa usimamizi mzuri walioufanya na kutoa wito wa utunzwaji wa miundombinu hiyo ili iweze kusaidia vizazi vingi.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Mgombe, Zabron Kigwe amesema kuwa uwepo wa shule hiyo utapunguza adha ya watoto kutembea umbali mrefu pamoja na vishawishi wanavyokumbana navyo njiani hasa kwa watoto wa kike pamoja na kutoa ahadi ya kuhakikisha shule inakuwa bora ili wanafunzi waweze kutimiza ndoto zao.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walioongea na mwandishi wetu wamemshuru Mhe. Rais kwa kufanikisha ujenzi wa shule hiyo kitu wanachoamini kitasaidia kwakiasi kikubwa maendeleo ya Kijiji cha Mgombe siku za mbeleni.


## TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# Wakulima wafagilia Ruzuku ya pembejeo ya Dkt Samia



NA MWANDISHI WETU

KUFUATIA mabadiliko makubwa katika sekta ya Kilimo na hasa uwepo wa mkazo wa serikali ya Awa,mu ya Sita katika usambazaji wa pembejeo za kilimo pamoja na kutoa mbolea ya ruzuku kumeleta matumaini makubwa kwa wakulima, katika maeneo mengi ya Tanzania.

Gazeti hili lililopiga kambi katika Kijiji cha Amani Makolo, wilayani Mbinga Songea mkoani Ruvuma kimekutana na idadi kubwa ya vijana walioacha shuguli nyingine na kuanza kuwajibika katika kilimo wakiitaja kuwa ndiyo kazi itakayowafanya waweze kufikia ndoto zao.

Mwamko huo ulishawishi hata wafanyabiashara ya usafirishaji Bodaboda kujiunga na shuguli za kilimo, unatajwa kuwa umechochewa na mpango wa Serikali Awamu ya Sita kutilia mkazo katika kilimo na kuondoa changamoto ndogondogo zilizokuwa zikikatisha tamaa wakulima.

Matumaini hayo yalianza kurejea mwaka jana wakati wa kikao cha Bunge ambapo waziri wa Kilimo Hussein Bashe alipeleka bungeni makadirio yaliyorudisha matumaini kwao na hasa uwepo kwa mpangi mzuri wa usambazaji wa mbolea ya ruzuku.

Akiwasilisha makadirio hayo mwaka jana Waziri wa Kilimo Hussein Bashe ameeleza kuwa, uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 uliongezeka na kufikia tani 20,402,014 ikilinganishwa na tani 17,148,290 katika msimu wa kilimo wa 2021/2022.

Alisema, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 19 katika kipindi tajwa ambapo uzalishaji wa mazao ya nafaka ulikuwa ni tani 11,448,757 ikilinganishwa na tani 9,233,298 msimu wa kilimo 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 23.9 na uzalishaji wa mazao yasiyo nafaka ulikuwa tani 8,953,258 ikilinganishwa na tani 7,914,992 katika msimu wa kilimo 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 13.1.

Waziri Bashe alieleza hayo wakati akiwasilisha bungeni hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za wizara ya kilimo kwa mwaka 2024/2025 mnamo tarehe 2 Mei, 2024.

Alisema, uzalishaji wa chakula kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani 16,390,404 kwa mwaka 2023/2024 na kuwepo kwa ziada ya tani 4,011,611 na hivyo, Taifa kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 124 ikilinganishwa na utosheleevu wa asilimia 114 mwaka 2022/2023.

Waziri Bashe alieleza kuwa pamoja na uwepo wa sababu nyingine zilizopelekea ongezeko hilo ni upatikanaji wa mbolea inayotolewa kwa wakulima kwa ruzuku.

Alisema, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 upatikanaji wa mbolea umefikia tani 1,052,218.4 ikilinganishwa na tani 819,442 mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 123.95 ya makadirio ya mahitaji ya mbolea ya tani 848,884 kwa mwaka.

Aidha, Waziri Bashe alibainisha kuwa, tani 471,839.9 zenye thamani ya ruzuku ya Shilingi 136,495,898,332 zimesambazwa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku ambapo tani 92,134.65 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.7 zimetolewa kama ruzuku kwenye zao la tumbaku.

Ameongeza kuwa, ili kurahisisha usambazaji wa mbolea kwa wakulima nchini, Wizara ya Kilimo imeongeza idadi ya waingizaji wakubwa wa mbolea kutoka 28 mwaka 2022/2023 hadi 31 mwaka 2023/2024; mawakala wadogo 3,265 mwaka 2022/2023 hadi 3,500 mwaka 2023/2024; na kusajili vyama vya ushirika 776 kwa ajili ya kuwa mawakala wa kusambaza mbolea za ruzuku kwa wakulima.

Vilevile Waziri Bashe alisema, ili kuwa na uhakika wa takwimu na taarifa za wakulima zitakazoiwezesha Serikali kuwa na mipango sahihi ya kuendeleza kilimo nchini; Wizara kupitia TFRA imepanga kuendelea na usajili wa wakulima katika mfumo wa kidigiti; kutoa mafunzo ya ukaguzi wa ubora wa mbolea; kusajili aina mpya za mbolea na visaidizi vyake 85; na kutoa leseni 2,100 za biashara ya mbolea.

Alisema hadi Aprili, 2024 wakulima 3,910,556 wamesajiliwa kwenye kanzidata https://ruzuku.tfra.go.tz na kueleza usajili huo utakamilika kwa kuchukua majira nukta (coordinates (GPS) za mashamba ya wakulima wadogo na baadaye mkulima kupatiwa hati ya shamba lake.

Waziri Bashe alibainisha kuwa, kwa mwaka 2024/2025 Wizara itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea na viuatilifu kupitia mpango wa ruzuku kwa mazao yote na kubainisha kuwa kupitia TFRA, Serikali itaratibu uingizwaji wa tani 1,086,115 za mbolea na kuzisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku utakaoendelea hadi mwaka 2025/2026.

Pia alisema Wizara itakamilisha vigezo muhimu katika mfumo wa usajili wa wakulima huku ikisajili wakulima, waagizaji na wasambazaji wa mbolea katika mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuimarisha usambazaji wa mbolea nchini.

Akizungumza kuhusu Kampuni la Mbolea Tanzania (TFC) alisema itanunua tani 100,000 za mbolea na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku.

Pamoja na hayo, TFC kwa kushirikiana na Kampuni ya Serikali ya Morocco (OCP Group Africa) itajenga kiwanda cha kuchanganya mbolea (Bulk Blending Facilities) chenye uwezo wa kuchanganya tani 120 za mbolea kwa saa kitakachochanganya mbolea kwa kuzingatia afya ya udongo ya eneo husika na hivyo wakulima kupata mbolea kuingana na mahitaji ya udongo.

Alisema, ili kuwezesha upatikanaji wa mbolea kwa wakulima karibu na maeneo yao na kwa wakati, kwa mwaka 2024/2025 Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na TFRA itaendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuwa Mawakala wa kusambaza mbolea kwa mpango wa ruzuku.

# TAHARIRI

## Kila la kheri Mkutano wa Nishati Afrika

JANUARI 27, 2025, mkutano muhimu wa Nishati unaowakutanisha Mawaziri wa Nishati, Mawaziri wa Fedha, na wadau wa maendeleo ulianza kufanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere Jijini la Dar es Salaam, Tanzania.

Mkutano huu, unaojulikana kama "Mission 300", unalenga kujadili mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa watu milioni 300 Barani Afrika.

Viongozi mbalimbali, wakiwemo Wakuu wa Nchi za Afrika, wanahudhuria mkutano huu.

Mawaziri wa Nishati 60 wanashiriki katika mkutano huo ambao jana ulifunguliwa na Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko.

Aidha leo ni siku ya kupata kauli mbalimbali kutoka kwa wakuu wa nchi, Sisi Jamvi la Habari tunautakia kila la heri Mkutano huo.

Tunafahamu kwamba, kwa muda mrefu suala la Watanzania kubadilika na kuachana na matumizi ya Nishati chafu, limekuwa ni jambo lililomo moyoni kwa kiongozi wa nchi Dkt Samia, hivyo hii tunaona kama ni hatua ya mbele kuelekea katika ndoto yake ya kuona mabadiliko haya.

Kadhalika tunatoa pongezi kwa Serikali ya Tanzania kwa kupata heshima kubwa ya kuwa mwenyeji wa mkutano huu, tunaamini kuwa amani iliyopo utulivu pamoja na mahusno mazuri na nchi jirani ndiyo matunda yake haya.

Ni wakati mzuri sasa wa kuhakikisha ile kauli ya mgeni njoo mwenyeji apone inatumika vizuri kwa kutangaza mambo mazuri ambao wageni wanaeweza kuvutiwa nayo, ikiwemo masuala ya utalii ambayo kwa sasa nchi imepiga hatua.

Tunaungana na Watanzania wote hususan wakazi wa Jiji la Dar es salaam kuwakaribisha wageni wetu na pindi watakapoondoka tutawasindikiza kwa upendo ili waikumbuke nchi yetu ya amani, pindi watakapokuwa katika nchi zao.

Tuna imani kubwa kuwa ujio wa wageni hawa umetuletea mabalozi watakaoitangaza vizuri nchi yetu kwa yale mema waliyokutana nayo. Mungu Ibarikmi Tanzania.

## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778,
- 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684,
- 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) (Kushoto), akisalimiana na Rais wa Benki ya Dunia, Bw. Ajay Banga, kando ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Afrika, ulioanza tarehe 27 Januari 2025 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Cha Julius Nyerere (JNICC), Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo unaotarajiwa kutamatika tarehe 28 Januari 2025 utawakutanisha Wakuu wa Nchi za Afrika na wadau muhimu wa sekta ya nishati ili kujadili mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya uhakika, nafuu, na endelevu kwa maendeleo ya Bara la Afrika.*

UCHAMBUZI

# Hizi ndiyo nchi zinazoshiriki Mkutano Nishati Afrika Jijini Dar es Salaam

NA MWANDISHI WETU

MKUTANO Mkuu wa Nishati unaendelea leo ukifikia siku ya pili tangu ulipoanza jana, huku ugeni mzito wa Marais wa matifa 25 iukitua katika ardhi ya Tanzania na kupokelewa na mwenyeji wao Rais wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan.

Licha ya viongozi hao wa nchi pia ugeni huo umejumuisha wakuu wa taasisi mbalimbali za Afrika pamoja na mawaziri wa Kisekta pamoja na wadau wengine muhimu waliokuwemo katika itifaki za mkuytano huo.

Wengineo ambao pia ni watoa mada ni Makamu wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) anayeshughulikia masuala ya nishati na mabadiliko ya hali ya hewa, Dk Kevin Kariuki amesema zaidi ya marais 25 na mawaziri wa fedha na nishati 60 wa Afrika watashiriki mkutano wa nishati utakaofanywa Dar es Salaam Januari 27 hadi 28, mwaka huu.

Aidha, viongozi wengine wa kimataifa watashuhudia wakuu wa nchi za Afrika wakikubaliana kusaini Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika, awamu ya kwanza utakaozishirikisha nchi 14.

Nchi hizo ni Tanzania, Malawi, Chad, Nigeria, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Niger, Liberia, Msumbiji, Madagascar, Zambia, Mali, Ivory Coast na Mauritania.

Alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mkutano huo unad[1]haminiwa na Benki ya Dunia, AfDB na washirika wengine wa maendeleo kuhakikisha watu milioni 300 Afrika wanafikiwa na umeme ifikapo mwaka 2030.

Dk Kariuki alisema mkutano huo ni muhimu kwani utakutanisha wakuu wa nchi na viongozi wengine ambao baada ya kujadiliana, watasaini Azimio la Dar es Salaam linaloweka makubaliano yaliyofikiwa kutekelezwa kuhusu mkutano huo muhimu.

"Hadi sasa marais zaidi ya 25 na mawaziri wa fedha na nishati zaidi ya 60 wa Afrika wanaku[1]tana hapa na tutashuhudia viongozi hao wakikubaliana na kuingia mkataba wa kuwezesha lengo la kusambaza umeme kwa watu milioni 300 kabla ya 2030 kufikiwa," alisema Dk Kariuki.

Alisema Benki ya Dunia na AfDB, Aprili mwaka jana walikubaliana kuwa haiwezekani wananchi wa Afrika wakaendelea kuishi katika upungufu wa umeme hivyo wakaamua kuja na mpango huo wa kuziwezesha nchi hizo kusambaza umeme kwa takribani wananchi milioni 300.

Alisema makubaliano hayo yanasimamiwa na nguzo kuu tano ambazo ni kuongeza uzalishaji na ku[1]wekeza katika miundom[1]binu kwa kuzingatia ush[1]indani, kuongeza miradi ya muunganiko wa mataifa ili kupunguza gharama za kusafirisha umeme.

# lugha, hisabati, sayaMkutano w

NA MWANDISHI WETU

TOFAUTI na ilivyokuwa siku za kawaida, jana Jumatatu na leo Jumanne Jiji la Dar es salaam unakofanyika Mkutano wa Nishati Afrika, kumekuwa kweupe huku msongamano wa watu na vyombo vya usafiri vikionekana kupungua kwa asilimia kubwa.

Hali hiyo imetokana na agizo la Jeshi la Polisi kufunga baadhi ya Barabara 9 zilizopo katikati ya Jiji kwa ajili ya kurahisisha wageni kutoka mataifa mbalimbali kuweza kuingia katika maeneo yatakayofanyika mkutano huo.

Jiji la Dar es Salaam jana lilianza kupokea takriban Marais 25, kutoka Mataifa mbalimbali ya Afrika pamoja na Mawaziri wasiopungua 60 watakakuwepo nchini kwa siku mbili kushiriki mkutano huo.

Licha ya katazo hilo la Jeshi la Polisi kutumia Barabara hizo za katikati ya Jiji pia Serikali ya mkoa wa Dar es salaam ulisitisha shuguli za kikazi kwa wafanyakazi wa serikali, ambao ulisababisha na wanafunzi pia kupumzika nyumbani kupisha ugeni huo.

Serikali iliwataka watumishi wa Umma kutulia majumbani na kufanyia kazi huko, isipokuwa wale ambao wanalazimika kuwepo katika vituo vya kazi.

Hali hiyo ilisababisha mji kuwa shwari, gazeti hili lilitembelea mitaa mbalimbali na kukutana na ukimya usiokuwa wa kawaida hasa eneo la Kariakoo ambako maduka machache yalifunguliwa huku Barabara zikiwa na purukushani chache sana tofauti na ilivyo siku za kawaida.

Kwa ujumla maeneo yote yaliyoainisha na Jeshi la Polisi wananchi wameitikia wito wa kutogusa na kufanyia shuguli zao maeneo ya pembeni ili kutii amri hiyo.

Mkutanoi huyo unatarajiwa kufunguliwa na Mwenyekiti wake Dkt samia Suluhu Hassan Rais wa Tanzania, ambapo ajenda kuu ikkiwa ni Afrika kutumia nishati safi.

Katika siku ya kwanza mkutano huo jana ulitanguliwa na mada zilizotolewa na Mawaziri wa Kisekta na kesho Wakuu wa nchi watatoa mada akiwemo Rais Dkt Samia.

Kwa Tanzania kuwa mgeni wa mkutano huo una faida kubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo nishati na utalii.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt.Doto Biteko amesema Mkutano huo una




lengo la kuharakisha upatikanaji umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo 2030 (Mission 300) utakaofanyika tarehe 27 na 28 Januari jijini Dar es Salaam yamefikia asilimia 95.

Dkt. Biteko amesema hayo tarehe 15 Januari 2025 mara baada ya kukagua maandalizi ya Mkutano huo katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam akiwa ameambatana na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila.

Amesema Wakuu wa Nchi 54 kutoka Bara la Afrika wanatarajiwa kushiriki pamoja na viongozi wengine ambao ni Mawaziri wa Fedha na Nishati kutoka barani Afrika, Marais wa Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), pamoja viongozi kutoka Jumuiya ya Ulaya na Jumuiya ya Umoja wa Afrika ambapo kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na kukamilisha ukarabati wa ukumbi wa JNICC.

“Kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na usajili na uthibitisho wa wageni ambao watakuja kwa ajili ya ushiriki na ukarabati wa maeneo mengine yatakayotumika kwenye mkutano huu, nichukue nafasi hii kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa hatua iliyofikiwa na kuliweka jiji kwenye mandhari ya kuvutia.” Amesema Dkt.Biteko

Ameongeza kuwa, Mkutano wa M300 umekuwa kivutio ambacho kimewashawishi Wakuu wa Taasisi nyingi za Kimataifa kuonesha nia ya kushiriki mkutano huo mkubwa katika Sekta ya Nishati.

Ameeleza kuwa, Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo kumetokana na Diplomasia nzuri ya Rais, Mhe. Dkt. San Suluhu Hassan ambayo imez kuimarisha uhusiano wa Tan nia kimataifa na kupelekea WB AfDB kuichagua Tanzania ku mwenyeji wa Mkutano.

Ametaja sababu nyingine Tanzania kuchaguliwa ku mwenyeji wa mkutano h muhimu ni mafanikio yaliyofi wa katika sekta ya Nishati hu akitoa mfano wa mafanikio kat usambazaji wa nishati vijijini.

Amesema vijiji vyote nch 12,318 vimesambaziwa umez na Vitongoji 34,000 kati ya 64,2

# wa Nishati walikausha Jiji la Dar



> Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,Albert Chalamila amesema maandalizi ya kupokea ugeni huo yako katika hatua za mwisho.

vilivyopo nchini, tayari vimesambaziwa umeme.

Ametaja baadhi ya faida za mkutano huo kuwa ni pamoja na kuongezeka idadi ya Watanzania watakaounganishwa na umeme ifikapo mwaka 2030 hadi kufikia milioni 13.5 kutoka milioni 5.2 ya sasa.

Ameongeza kuwa, katika mkutano huo nchi zitasaini mikakati ya kuharakisha kusambaza umeme kwa wananchi ambayo itaeleza kwa kina hatua gani zitachukuliwa chini ya mwavuli wa WB na AfDB. Ameongeza kuwa, faida nyingine zitakazotokana na mkutano wa M300 ni kuongezeka kwa fursa za uwekezaji, kuimarisha biashara na kuongeza heshima ya nchi katika Duru za kimataifa na Tanzania kuwa Taifa linalopigiwa mfano kwenye nyanja mbalimbali.

Dkt. Biteko ametoa wito kwa Watanzania kuupokea kwa mikono miwili mkutano huo ambao kwa kiasi kikubwa unazidi kumheshimisha Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Watanzania kwa ujumla.

Aidha, ametoa wito kwa wananchi kuendelea na hali ya amani na utulivu kuelekea katika mkutano huo wa kihistoria kutoka nchi ipige hatua kwenye Sekta ya Nishati kwani ni Mkutano Mkubwa wa kwanza kufanyika.

Vilevile ametoa wito kwa Waandishi wa Habari kuutangaza Mkutano huo kwa Watanzania ili waufahamu kwa kina na kufahamu fursa zilizopo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila amesema maandalizi ya kupokea ugeni huo yako katika hatua za mwisho.

Amesema ili kufanikisha mkutano huo, baadhi ya mitaa itafungwa ili kuwezesha maonesho na utalii wa ndani ikiwa ni pamoja na utalii.






# Miaka mitatu inayojibu uchapa kazi wa Dkt Samia



NA MWANDISHI MAALUM

KATIKA kipindi cha Miaka mitatu ya Uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sekta ya afya imepatiwa kiasi cha Shilingi Trilion 6.722 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele mbalimbali ili kuimarisha huduma za afya nchini ambapo Wizara ya Afya imetekeleza kwa mafanikio makubwa majukumu yake, ikijikita katika maeneo Makuu mbalimbali.

Utekelezaji wa majukumu haya unatokana na jitihada zinazofanywa na Rais Samia, kutokana na maono yake, utu na mapenzi mema ya kutaka kuona wananchi wake wanakuwa na Afya njema.

Kwa mujibu wa tovuti ya Wizara ya Afya imeeleza kuwa, kutolewa kwa kiasi hicho cha fedha, Wizara ya Afya imeweza kutekeleza Miradi kadhaa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia ambayo ni pamoja na Miundombinu ya kutolea Huduma za Afya nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya.

> "Kwa upande wa ngazi ya msingi, ujenzi wa majengo ya dharura (EMD) majengo 82 katika ngaziza Halmashauri unaendelea, ambapo EMD 66 zimekamilika na zinatoa huduma.

Upatikanaji wa huduma za Ubingwa na Ubingwa Bobezi nchini, kuimarisha huduma za Uchunguzi wa magonjwa ikiwemo huduma za Mionzi na kuimarisha Huduma za Afya ya Uzazi.

Huduma nyingine zilizoimarishwa ni huduma ya Mama na Mtoto, kudhibiti maambukizi ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Malaria na Magonjwa ya mlipuko, Ajira kwa Watumishi na Ufadhili wa Wanafunzi katika ngazi na fani mbalimbali pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.

Mbali na mafanikio hayo ya Sekta ya Afya katika Uongozi wa Rais Dkt. Samia, pia utekelezaji wa miradi hiyo uliwezesha kuongeza majengo ya Huduma za Dharura



(EMD) kwa kukamilisha ujenzi wa majengo 23 ya kutoa huduma za dharura (EMD) katika Hospitali Maalumu za Kanda na Mikoa na kuziwekea vifaa na vifaa tiba.

Aidha kwa upande wa ngazi ya msingi, ujenzi wa majengo ya dharura (EMD) majengo 82 katika ngaziza Halmashauri unaendelea, ambapo EMD 66 zimekamilika na zinatoa huduma.

Jitihada za Rais Samia, zimewezesha kupatikana kwa huduma za kipimo cha CT Scan zimeweza kupatikana katika Hospitali 27 kati ya Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa nchini ambapo kwa mwaka 2023, jumla ya wagonjwa 15,386 walipatiwa huduma za kipimo cha CT Scan katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, huduma ambazo hapo awali zilikuwa hazitolewi katika hospitali za Rufaa za Mikoa.

Maboresho haya katika Sekta ya Afya, yamewasaidia wananchi kupata huduma bora za tiba na vifaa tiba, kwa muda mfupi na hivyo kusaidia kuokoa maisha

# MTAMA, ZAO LINALOTIBU MARADHI YA UZEE



NA MWANDISHI WETU

MAMILIONI ya watu duniani hupoteza maisha kwa sababu ya magonjwa ya moyo, saratani na uzee. Kwa ugonjwa wa saratani pekee, Shirika la afya duniani (WHO) linakadiria kuwa kufikia mwaka 2030 utapoteza maisha ya watu zaidi ya 1.1milioni barani Afrika kama hautadhibitiwa. Lakini sasa huenda idadi ya vifo hivyo na vifo vitokanavyo na magonjwa ya moyo na uzee ikapungua kwa matumizi ya mtama hasa wa kahawia. Kituo cha Utafiti wa kilimo, TARI-Ilonga, nchini Tanzania kimegundua mbegu za mtama 'inayoweza kupunguza magonjwa kama ya saratani, kisukari, magonjwa ya moyo na kupunguza kasi ya uzee'.

Mtama ni zao muhimu la chakula lakini lisilopewa sana umuhimu katika nchi ya Tanzania, pengine kutokana na jamii yake nyingi kutokuwa na mazoea ya kula vyakula vinavyotokana na zao hilo.

Ni zao hilo la mtama linaloonyesha kustamili ukame na linaloweza hata kustawi maeneo yenye ukame na kusaidia jamii kupata chakula lakini kilimo chake bado kimekuwa cha kawaida kisichooneka na kutiliwa mkazo kama mazao mengine ya chakula na biashara.

Wakulima wengi wa Tanzania wanalitazama zao hili kama ni nyongeza ambapo mkulima anaweza kulima mazao mengine ndani ya shamba lake, kisha akatafuta eneo dogo kwa ajili ya kuotesha mtama ambao utatumika kwa matumizi madogo kama vile utengezaji wa pombe na kutumiwa kwa kikasi kidogo kama chakula.

Unga wa mtama licha ya ubora wake na kuthibitika kuwa ni tiba ya maradhi mengi lakini hakuna jamii inayoonekana kutilia maanani, kilimo chake.

Kwa wanaotambua umuhimu wa zao hili hulitilia mkazo sana, kwani ni zao linaloanza kutumika kabla ya kukomaa ukitoa chakula kizuri na chenye protini za kutosha ambao baadhi ya makabila wanakiita Msima.

Msima ni mtama mbichi ambao bado hajakomaa ambao mara nyingi hutumiwa kulowekwa kwenye maji na kuwekwa viungo vichache na kuliwa ukiwa mbichi, ambapo hutoa aina ya tuwi kama maziwa ambalo kwa asili ni chakula muhimu na tiba.

Kizazi cha enzi hizo kilitumia aina hiyo ya chakula kwa ajili ya kusaidia mmengenyo wa chakula tumboni, hasa kuondoa gesi na Tindikali iliyozidi tumboni ambayo hivi sasa umekuwa ni ugonjwa mkubwa unayoitesa jamii.

Msima unapotafunwa vizuri na kumeza tui lake haichukui hata dakika tano, tumbo huanza kupata aina ya asidi inayokimbiza ile iliyojaa kwenye maeneo ya tumbo na kumpa nafuu kubwa mwenye tatizo hilo.

Zao hilo pia limekuwa likisaidia kuzibua mirija hasa kwa akina mama wanaosumbuliwa na shida ya kuziba mirija ya kizazi, Msima ulitumiwa na kizazi cha enzi hizo kutibu wasichana wanaoonekana kukosa kizazi au kupata mabadiliko ya hedhi yasikuwa ya kawaida.

Kupitia zao hilo baadhi ya wazee waligundua faida zake waliweza kupata umaarufu mkubwa kutokana na kusaidia jamii zenye matatizo mbali mbali, inaeelezwa kuwa ziliwahi kutokea mbinu za kuficha ukweli kuhusu tiba ya Mtama ili waliogundua waendelee kujitengenezaea sifa ya kutoa tiba.

Mfano mtaalamu aliyegundua tiba ya Mtama kupitia aina hiyo mbichi ya Msima, yeye aliiboresha kwa kuchanganya na mizizi mingine ili zao hilo lionekane kama kiungo tu ili kuficha utambuzi kwa mteja wake na hivyo kuendelesa kujipatia sifa na faida.

Licha ya taasisi za utafiti kulitaja zao hilo na kueleza faida zake katika tiba lakini inaonyesha bado nao wamelidharau kwa kulifanyia namna bora zaidi ya kulifanyia utafiti wa kina, vinginevyo wangegundua faida zaidi ya hizi maarufu zilizotangazwa.

# Nishati ya umeme yaifungua Bagamoyo

NA MWANDISHI WETU

VIJIJI na vitongoji kadhaa wilayani Bagamoyo mkoa wa Pwani vili vkuwa giza kutokana na kutopata nishati ya umme, vingine tangu ulipopatikana uhuru wa nchi hii mwaka 1961, lakini sasa maeneo mengi wanatos shukurani kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwezesha kuondoa changamoto hiyo.

Mfano ni Kijiji cha Saadan kilichokuwa katikati ya Hifadhi hiyo ambacho awali iliyogubikwa na giza, umasikini uliochagizwa ukosefu wa huduma za kijamii na kulifanya eneo hilo lisifikike kwa urahisiu kutokea katika miji mikubwa inayolizunguka kama vile yalipo makao makuu ya wilaya, Bagamoyo na Jiji la Dar es salaam.

Nyuma ya miaka ya 1960 hakukuwa na mwanga katika eneo hilo, wenyeji walioshi eneo hilo walijikita katika kazi ya uvuvi wakitumia nyenzo duni, pia kulikuwa na biashara nyingine kama vile ukataji wa ukindu, zao lililotumika sana kwa ajili ya ususi wa mikeka na vikapu, kadhalika ukataji miti ya Mikoko iliyokuwa ikisafirisahwa kwa majahazi kwenda katika miji ya Zanzibar na hata nje ya nchi Mombasa na Visiwa vya Comoro.

Mwanga ulijitokeza mwaka 1962 ilipoanzishwa Bustani ya wanyama, iliyojmumuisha wanyama wachache waliofungiwa katika Ng'enge (Zoo) kubwa na ndogo, zilizoanza kuvuta macho ya watalii kuanza kutembelea kijiji hicho kilichokuwa na wakazi wachache, wengi wao wakitokea maeneo mbalimbali ya nchi na kuafauata biashara ya uvuvi.

Enzi za Ukoloni Saadani iliwahi kukaliwa na Koloni la Waarabu walioendesha biashara ya utumwa, iliyotanabaishwa na kuwewpo mabaki ya magofu machache yaliyokuwa yakitumiwa katika biashara hiyo, pia gati kuu la kusafirishia watumwa kutoka bandari ndogo ya Saadani kuelekea Unguja na nchi nyingine za jirani.

Kwa mujibu wa simulizi za wazee wa mji huo hata jina hili la Saadani, lilitokana na Mzee mmoja wa Kiarabu aliyekuwa akimiliki saa ya ukutani, hivyo alipochoshwa na maswali ya kuulizwa muda "Saa ngapi? kila mara akawa anawajibu "kama unataka saa nenda kaangalie ndani.

Kwa vile hakuweza kutamka vizuri maneno ya Kiswahili ndipo alipokuwa akikatisha tu kwa kusema "Saadani" ndipo likazaliwa jina hili.

Ukuaji wa mbuga hiyo ya wanyama iliweza kuupa umaarufu mji huo mdogo ulipo kandoni mwa Bahari ya Hindi kwa kuanza kutembelewa na watalii pamoja na watu maarufu, akiwemo Mwanasiasa aliyeshika nyadhifa mbalimbali serikalini Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyefika Saadani Mwaka 1974 na kuweka jiwe la Msingi la kumbukumbu ya ujiuo wake na uzinduzi wa bustani hiyo ya wanyama.

> ***Kufuatia kupatikana kwa nishati hiyo kijiji cha Saadan kilichokuwa kikikumbana na matukio ya kuvamiwa na wanyama wakati na waharibifu kama vile Tembo na Simba sasa imepungua na kuwa sehemu salama toka kijiji hadi mmbuga yenyewe.***

Kwa bahati nzuri kijiji cha saadan kiliweza kuonja maendeleo mapema kwa kupata zahanati pamoja na Shule ya Msingi iliyoanza ikiwa na madarasa manne na baadaye ikaendelea na kukamilisha madarasa yote saba, pia kiliwahi kununua gari aina ya Center kwa ajili ya shughuli za kijiji.

Kupitia uwepo wa bustani hiyi ya wanyama kijiji nhicho kilianza kupokea wafanyakazi wengi wakati huo wakijulikana kama 'Game Scout' kutoka maeneo mbali mbali na baadhi waliajiriwa wananchi wakazi wa kijiji hicho na vile vinavyozunguka bustani hiyo kama Uvinje, Buyuni Kuu na Buyuni Kitopeni.

Kwa kuwa mazingira ya hifadhi ya Saadani ni Jangwa wafanyabiashara wenye asili ya India chini ya Kampuni ya Albhai Panju and Sons walianzisha kilimo cha zao la chumvi na kuvuna maelfu ya tani waliyoisafisha kwenda maeneo mbalimbali ya nchi.

Kampunu hiyo iliweka kiwanda chake maeneo ya Malumbi nje kidogo ya Bustani ya Wanyama ya Saadan, na baadaye serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa (Stamico) iliweza kuanzisha kiwanda cha kisasa cha uzalishaji chumvi na kupeleka watalaamu wa madini na kuanzisha mradi huo uliokuwa mkubwa sana.

Lakini katika kipindi chote Hifadhi hii iliyopo chini ya TANAPA, iliyoanzishwa mwaka 1962 ikiwa ni pori la akiba na Mwaka 2005, kupandishwa hadhi rasmi na kuwa hifadhi ya taifa, ikashuhudia ongezeko la wahamiaji waliovutwa na upatikanaji wa Samaki aina ya Kamba ambao katika kijiji hicho hujulikana kama Makaji ambayo yalikuwa yakiuzwa kwa bei kubwa na kuwa na maslahi mazuri kwa wavuvi.

Makampuni binafsi kama vile Dar Ocean Product na hata Tafico walikivamia kijiji hicho kwa ajili ya kununua samaki hao kutoka kwa wavuvi wenyewe moja kwa moja.

Lakini katika kipaindi chote hivyo huku zikipita awamu zote tano la utawala wa Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania wana kijiji walikuwa na changamoto mbalimbali za maendelo kama vile ukosefu wa nishati ya umeme na maji.

Kadhalika miundombinu ya barabara inayotokea mwishoni mwa daraja la kisasa la Wami kuingia kulia katika Vijiji vya Mandela na baadaye Miono, Zimbili, Mkange na kuingia Saadan ilikiuwa ipo katika hali mbaya.

Serikali ikaifanyia kazi changamoto hiyo baada ya kufanya ujenzi wa kisasa wa baraba inayotokea eneo la Makurunge Bagamoyo yalipokuwa mashamba ya mifugo ya Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo (RAZABA) hadi kuingia Kijiji cha Saadani kupitia miji iliyokuwa kandoni mwa bahari ya Hindi kama vile Mkwaja na Buyuni.

Katika utawala huu wa awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, Mbunga ya Saadani inang'aa,baada ya kupatiwa umeme wa kutosha.

Kwa takriban mwaka sasa wakazi wa Saadani wanafaidika na uwepo wa nishati ya umeme, waliyoikosa tangu nchi kupata uhuru.

Kufuatia kupatikana kwa nishati hiyo kijiji cha Saadan kilichokuwa kikikumbana na matukio ya kuvamiwa na wanyama wakati na waharibifu kama vile Tembo na Simba sasa imepungua na kuwa sehemu salama toka kijiji hadi mmbuga yenyewe.


Hivi sasa mkazi wa Saadani atakayetafuta bughudha ya kukutana na wanyama ni yule atayekwenda misituni kwa ajili ya kufanya shuguli za kibinadamu kama vile kuzoa chumvi au kuvua katika maeno yasiyokuwa rasmi kwa shuguli hiyo.

Wakazi wa Saadani kwa sasa wanaliimba jina la Rais Samia kwamba ndiye aliyendika historia ya kuing'arisha Saadani, kizazi kipya kutoka eneo hili sasa hakina tena histoiria ya enzi hizo ambazo wakazi walifuata taa aina ya Karabai iliyokuwa ikiwashwa na wafanyabiashara maarufu enzi hizo Mohamed Mwarabu al maarufu Mzee Ganda na Mfaume Akida Mimi na Sheikh Said waliokuwa wakimiliki maduka zama hizo.



# TRUMP AENDELEA KUINYIMA USINGIZI URUSI

NA MWANDISHI WETU



KUREJEA madarakani kwa Donald Trump, ambaye hapo awali aliahidi kumaliza vita nchini Ukraine, kumeibua hali mpya ya wasiwasi miongoni mwa makampuni ya Magharibi ambayo bado yanaendelea kufanya shughuli zake nchini Urusi.

Hali hii inatokea wakati serikali ya Urusi ikiendelea kuimarisha sheria na masharti yanayoongeza gharama za kujiondoa kwenye soko lake, pamoja na kutoa vivutio finyu kwa wanaotaka kuendelea kufanya biashara nchini humo.

Tangu Moscow ilipoivamia Ukraine mnamo Februari 2022, makampuni makubwa kama Renault, McDonald's na Heineken yaliondoka Urusi, yakiuza hisa na mali zao kwa hasara kubwa kufuatia sheria kali zilizowekwa.

Baadhi ya makampuni mengine, hususan yale ya vyakula na bidhaa za usafi kama PepsiCo, Procter & Gamble na Mondelez, bado yanaendelea kufanya shughuli zake nchini Urusi kwa kile wanachokiita "sababu za kibinadamu."

Benki kadhaa za Ulaya kama Raiffeisen Bank International na UniCredit nazo zinajikuta katika mtanziko huohuo, zikikabiliwa na ugumu wa kurejesha mali zao zilizozuiliwa nchini Urusi.

Tayari, serikali ya Moscow inadai punguzo la angalau asilimia 60 wakati wa miamala ya kuondoka, sambamba na 'mchango wa hiari' wa asilimia 35 kwenye bajeti yake, ambao Marekani imeuita "kodi ya kuondoka."

Je, Trump atafanya nini?

Wadau mbalimbali wa kibiashara na kisheria, akiwemo Ian Massey, mtaalam wa biashara, wanasema ushindi wa Trump unaongeza sintofahamu kwa mashirika yenye mali au vitegauchumi nchini Urusi.

Kremlin inatarajiwa kuendelea kuongeza gharama za kujiondoa ili kufidia hasara, huku Trump akitabiriwa kupunguza gharama za uendeshaji kwa makampuni yanayopendelea kuwekeza au kurejea Marekani.

"Inatarajiwa itachukua miezi kadhaa kuumaliza mzozo wa Urusi na Ukraine, hata kama Trump ataingilia kati," anasema Massey. "Hivyo, makampuni yatakuwa yakitathmini mikakati yao kwa umakini zaidi."

Baadhi ya wachambuzi wanaamini kurejea kwa Trump kunaweza kuwapa uwezekano mpya makampuni yanayotaka kuendelea na biashara zao Urusi, ikiwa vikwazo vya kimataifa vitaregezwa. Kwa upande mwingine, huenda yakatokea mazingira yatakayoharakisha makampuni mengine kukamilisha mpango wao wa kujiondoa kabisa.

Sheria za Moscow zinavyozidi kuwa kali

Kwa mujibu wa Alexei Yakovlev, mkurugenzi katika Wizara ya Fedha ya Urusi, mazungumzo ya mikataba ya kuondoka kwa makampuni fulani bado yanaendelea.

Hata hivyo, hakufafanua ikiwa kurejea kwa Trump kunaweza kuzuia hatua za makampuni hayo au kusaidia mengine kurejea nchini Urusi.

Serikali ya Urusi imesisitiza kuwa mpango wowote wa kujiondoa unaohusisha dola milioni 488 au zaidi, lazima upitishwe na Rais Vladimir Putin.

Aidha, wanunuzi wa ndani wanaotaka kununua mali za makampuni ya nje, wanapaswa kuonyesha mkakati mahsusi, likiwemo jinsi gani kununua au kutonunua biashara husika kunavyoweza kuathiri uchumi wa Urusi.

Mustakabali uliojaa sintofahamu

Mengi yamebadilika tangu mwaka 2022, wakati makampuni mengi yalianzisha mazungumzo ya kujiondoa. Kwa sasa, mchakato huo ni mgumu zaidi kutokana na:

Tathmini ya Thamani: Thamani ya makampuni inahitajika kuthibitishwa na wataalam huru wanaoteuliwa na Wizara ya Uchumi ya Urusi.

Minada ya Uwazi: Serikali inaendesha minada ili kuwapa wanunuzi wote wa ndani fursa sawa, jambo linalowapa makampuni ya Magharibi hofu ya kushindwa kupata bei nzuri.

Kurejea kwa Trump madarakani kumebadili kabisa ramani ya kisiasa na kiuchumi, na huenda kukabadilisha mwelekeo wa makampuni ya Magharibi yanayoyumba kati ya kuondoka au kuendelea kubaki Urusi.

Hata hivyo, mwelekeo huu unatabiriwa kuambatana na mifumo mipya ya kisheria inayodhibiti mtiririko wa rasilimali na fedha.

Bado hakuna uhakika juu ya lini vita vya Ukraine vitakoma, au jinsi Trump atakavyoshughulikia mgogoro huo na vikwazo dhidi ya Urusi.

Wakati uamuzi wa mwisho ukisubiriwa, makampuni ya Magharibi yanajikuta kwenye maamuzi magumu zaidi kuliko wakati wowote ule.


Je, yatadumu Urusi, kuondoka sasa, au kusubiri kuona iwapo sera za Trump zitapunguza gharama zao za uendeshaji na athari za vikwazo?

Ni wazi kuwa mustakabali wa uchumi wa kimataifa unazidi kugubikwa na hali ya kutokuwa na uhakika, huku macho ya wachumi na wafanyabiashara wengi yakielekezwa kwenye Ikulu ya Marekani na Kremlin.



# Michezo Kimataifa


## Tetesi za soka



MANCHESTER United wameomba kufahamishwa kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, huku winga wa Argentina Alejandro Garnacho, 20, akihusishwa na uhamisho wa kwingineko.



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.




1

MSHAMBULIZI wa Manchester United Marcus Rashford, 27, yuko tayari kupunguziwa mshahara katika jaribio la kutaka kuhamia Barcelona mwezi Januari. (Daily Star Sunday)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani






# FADLU AENDESHA TIZI LA NGUVU SIMBA SC

NA MWANDISHI WETU

KOCHA Mkuu wa Simba Fadlu Davis ameendelea kuwapa mazoezi ya nguvu wachezaji wake huku akiongeza mbinu za kuunganisha kikosi ili kicheze kitimu, tayari kwa ajili ya kushiriki michuano ya hatua ya Robo Fainali ya Kombe la Shirikisho pamoja na Ligi Kuu ya Tanzania.

Kocha huyo Raia wa Afrika Kusini amesema anafanya hivyo kutokana na ukweli kwamba kikosi chake hakina mapungufu ya mchezaji wa eneo fulani, bali kinachotakiwa ni kuwafanya wacheze kitimu, hivyo ana kazi kubwa ya kutafuta muunganisho wa kikosi chake.

Hiyo imetokana na kile alichodai kwamba usajili wao ulizingatia kila eneo, huku Kamati iliyofanya kazi hiyo ikijaribu kupata wachezaji wazuri kutoka timu mbalimbali, ambao walihitaji kuwaunganisha, zoezi ambalo linakwenda vizuri.

Katika mkakati huo Fadlu amewahakikishia mashabiki wa Simba kuwa kiungo wao hatari Elie Mpanzu katika mechi zijazo wataanza kumuona akianza kikosi cha kwanza kutokana na kuzoea na kupata pumzi ya kutosha tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Mpanzu alikuwa akitumiwa sana kucheza dakika chache za mwanzoni au mwisho, ambapo sasa ataonekana akiongezewa muda wa kuitumikia timu yake hiyo aliyoijiunga nayo akitokea AS Cita ya nchini DRC.

# Burudani



## Msondo Ngoma wamwimbia Dkt Samia

NA MWANDISHI WETU

BENDI kongwe ya muziki wa dansi Msondo Ngoma wiki hii imemaliza mazoezi ya wimbo maalum waliouandaa kwa ajili ya kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, wimbo huo ambao umeanza kupingwa katika maeneo mbalimbali inapofanya maonyesho yake ya wiki, umeanza kuwa kivutio kwa mashabiki.

Akizungumza na gazeti hili Meneja wa bendi hiyo Saidi Kibiriti alisema, hao kama Tasisi wameona juhudi za makusudi zinazofanywa na kiongozi huyo na kuona ipo sababu ya kumpa maua yake.

Naye mkuu wa Jukwaa wa bendi hiyo Juma Katundu alisema kuwa katika wimbo huo wanazungumzia baadhi ya manufaa waliyopata Watanzania katika kipindi cha Utawala wa awamu ya sita kama vile ujenzi wa reli ya kisasa pamoja na usafiri wa Treni ya umeme, pia miundombinu na ukuaji wa uchumi mambo ambayo kwa sasa yanaonekana hata kwa macho.

Alisema wimbo huo utakapokamilika watairekodi na kisha kuusambaza katika vituo vya redio na Televisheni ili Watanzania waone kazi hiyo iliyolenga kutoa wasifu na kuzitambua juhudi zinazofamnywa na viongozi katika mikakati ya kuendeleza taifa la Tanzania.

Alisema huo ni mwanzo lakini bendi hiyo itakuwa ikitunga nyimbo kama hizo kwa ajili nya viongozi mbalimbali na hata watu wengine wanaojitolea kusaidia masuala ya kijamii katika nchi hii.

## Jb atamani waigizaji wapya

NA ERYNE BANDA

MSANII mkongwe wa Bongo Movie, Jacob Steven 'JB', amesema sababu za maprojuza kurudia wasanii wale wale kwenye filamu na tamthilia ni kutokana na uwepo wa waigizaji wachache wenye uwezo huo.

JB alisema atamani wapate waigizaji wapya wenye uwezo mkubwa zaidi, ndiyo maana yuko bize kufanya usaili wa waigizi wapya ili kuleta sura mpya kwenye uigizaji kwani mashabiki wamechoka kuona waigizaji ni wale wale hawabadiliki.

"Mashabiki wasitulaumu sana kwa maprojuza kurudia wasanii wale wale kwenye filamu na tamthilia. Sababu ni tasnia ya uigizaji ina waigizaji wachache wenye uwezo wa kuigiza. Ndiyo sababu mashabiki wanaona hawabadiliki.

Binafsi nimeligundua hilo na natamani nipate waigizaji wapya wenye uwezo mkubwa zaidi, ndiyo maana niko bize sasa hivi kufanya usaili wa waigizi wapya ili kuleta sura mpya kwenye uigizaji," alisema JB.





## Belle 9 ammwagia sifa Ben Pol

NA EMMANUEL TAIRO

STAA wa RnB Bongo, Abednego Damian 'Belle 9', ameweka wazi kuwa, katika utaratibu wake wa kufanya kazi haangalii wala kuchagua wa kufanya naye.

Belle 9 ambaye aliwahi kutamba na ngoma ya 'Sumu ya Mapenzi "Najua watu huwa tunasahau fadhila na mimi kiukweli nisiwe mchoyo wa kutoa shukurani, ninamshukuru sana, Ben Pol kwa mambo aliyoweza kunifanyia mpaka hapa nilipofikia.

"Alikuwa mwalimu mzuri sana kwangu na alikuwa anapenda nitimize ndoto zangu, hakutaka nikate tamaa kabisa," anasema Belle 9

Mwimbaji huyo ameliambia Gazeti la Jamvi la Habari kuwa, msanii anayejiamini kwenye kazi zake haoni sababu ya kuanza kuchagua watu wa kufanya nao kazi, bali kuona wasanii wachanga wanafika mbali.

## Mlela: Sanaa inatakiwa ikue

NA EMMANUEL TAIRO

MKALI katika tasnia za filamu, Yusuf Mlela amesema kutokana na mabadiliko yanayohitajika kwenye sanaa, haoni tatizo wasanii wa Bongo Fleva wakiingiza kwenye filamu na tamthiliya.

Akizunguza na mwandishi wa gazeti hili, Mlela ambaye ukiachilia mbali na uigizaji pia ni muongozaji wa tamthilia, amesema kuwa sanaa kila siku inatakiwa ikue ndiyo maana wasanii wengi wa Bongo Fleva wameamua kufanya hivyo.

"Unajua sanaa inatakiwa ikue kila siku mambo yanatakiwa mapya, ukiangalia sisi wote ni wasanii na msanii lazima aweze kuonyesha uwezo wake katika sanaa, acha waingie ili kuleta vitu vya tofauti," alisema Mlela.

JAMVI LA HABARI
SPOTI
JUMANNE JANUARI 28, 2025



## Noma Mjengo wa Mr Pimbi adai kuwezeshwa na Geo Devi

>> Soma Uk. 15

# FADLU AFAGILIA KASI YA SIMBA



NA MWANDISHI WETU

KOCHA Mkuu wa Simba Fadlu Davis amewapongeza wachezaji wake kwa kuongezeka kiwango cha Stamina na kuonyesha ukakamavu muda wote wa mchezo.

Kocha huyo licha ya timu yake kuichakaza Kilimanjaro Stars kwa jumla ya mabao 6-0, lakini amesema yeye alikuwa na kazi ya kufanya tathmini ya kila mchezaji kuangalia uwezo wake wa kuhimili dakika 90.

Pia ameeleza kufurahishwa na ushindi huo mnono wa michuano ya ASFA na kudai ndiyo dhamira ya timu yake msimu huu.

Kwa upande wake kiungo mkongwe katika kikosi hicho Mzamiru Yassin, amewasifu wachezaji wa Kilimanjaro akidai kuna baadhi ni wachezaji wazuri.

“Kuna mchezaji alivaa jezi namba 30 alikuwa mzuri sana na wengine kama watatu hivi” alisema.

Katika mchezo wa juzi Simba ilichezesha nyota wake ambao huko nyuma hawakupata nafasi nyingu za kucheza.

## Mtibwa yatoa neno kwa Simba, Yanga

NA MWANDISHI WETU

KLABU kongwe ya soka katika soka la Bongo Mtibwa Sugar, imezikumbusha klabu za Simba na Yanga kuikumbuka Klabu hiyo ya Turiani kwa vile ina mchango mkubwa Kwa maendeleo ya timu zao.

Hayo yamezungumzwa na Afisa Habari wa Klabu hiyo Thobias Kifaru alipokuwa akieleza mikakati ya timu hiyo kurejea Ligi Kuu, msimu ujao. Kifaru alisema Klabu ya Mtibwa tangu ilipoanzishwa na kuanza kuzalisha vipaji imekuwa ndiyo kimbilio la Simba na Yanga kuvuna wachezaji, lakini inapofanya vibaya Wala hawashituki.



Mtibwa iko katika nafasi nzuri ya kupanda daraja msimu ujao huku uongozi wake ukianza kurudisha wachezaji wa zamani katika benchi lake la ufundi.

“Muda huu tunaipambania timu irejee Ligi Kuu vigogo wa Simba na Yanga wako kimya, wanasubiri kuja kufumua kikosi kwa kuchukuwa wachezaji wetu” alisema.



## Aziz Ki ujanja wake upo hapa

**KIUNGO** mshambuliaji wa Yanga, Aziz Ki chaguo la kwanza la Kocha Mkuu, Sead Ramovic ujanja wake upo kwenye mguu wake wa kushoto ambao umekuwa na mashuti yenye nguvu kitaifa na kimataifa.

>> Inaendelea Uk. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM